

# Buriani Nkaissery

Kifo ninakulaumu, moyoni nakuchukia,  
 Kifo ninakushutumu, rafiki metuibia,  
 Kifo unatuhukumu, upesi bila hatia,  
 Kwaheri Nkaissery, metangulia mapema.

Metangulia mapema, mbele za haki jamani,  
 Tunaumia mtima, ulirudisha amani,  
 Ulikomesha zahama, rudi kweli twatamani,  
 Kwaheri Nkaissery, taonana kwa Manani.

Taonana kwa Manani, siku yetu ikifika,

Machochi tele machoni, mebaki kusikitika,  
 Wengi hatujaamini, kama kweli meondoka,  
 Kwaheri Nkaissery, mebaki mudomo wazi.

Mebaki mdomo wazi, kunena katu sitaki,  
 Usalama waziwazi, uliweza kuafiki,  
 Lidhibiti majambazi, kwa amani tukabaki,  
 Kwaheri Nkaissery, tutakupeza milele.

Tutakupeza milele, nyoyoni tunaumia,  
 Mejawa huzuni tele, Kenya twasikitikia,  
 Hatua lisonga mbele, Jahazi kishikilia,  
 Kwaheri Nkaissery, metuwacha taabani.

Josphat Cheruiyot  
 Chuo Kikuu cha SEKU, Kitu